Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | June-2026

EAJK

# Mageuzi ya Kimofolojia ya Msamiati wa Mame-Bantu kwenda Lugha za Kibantu: Mifano kutoka Kinyakyusa

**Author**

**Emanuel Deogratius**

**Author's email:** geydanema@gmail.com

**Institute of Adult Education, Dar es Salaam- Tanzania.**

**Cite this article in APA**

Deogratius, E. (2026). Mageuzi ya kimofolojia ya msamiati wa Mame-Bantu kwenda lugha za Kibantu: Mifano kutoka Kinyakyusa. *Eastern Africa journal of Kiswahili,* 5(1), 65-78. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.993

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-04-13
Accepted: 2026-05-25
Published: 2026-06-12

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Makala hii inahusu mageuzi ya kimofolojia kutoka Mame-Bantu (MB) kwenda Kinyakyusa. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza mabadiliko ya kimofolojia ya maumbo ya vitenzi na nomino kutoka MB kwenda lugha ya Kibantu. Utafiti huu ni wa kitaamuli na uliongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia ya Wolfgung U Dressler (1987). Data za utafiti zilikusanywa kwa njia ya uchambuzi wa matini pamoja na usaili wa wazungumzaji asilia wa Kinyakyusa. Jumla ya maumbo ya msamiati 35 ya MB yalichambuliwa kutoka kwenye matini ya Bostoen na Bastin (2016), kisha kufasiriwa kwa Kinyakyusa. Aidha, usaili uliofanyika kwa wazungumzaji asilia sita (06) wa Kinyakyusa ulilenga kupata tafsiri ya maumbo ya vitenzi na nomino zilizochunguzwa. Sampuli ya utafiti iliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa wa kipekee na kwa kuzingatia vigezo vya umri, jinsi na umahiri wa lugha. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwapo kwa mageuzi ya kimofolojia ya msamiati wa MB kwenda Kinyakyusa. Mageuzi haya yanachagizwa na mabadiliko ya vitamkwa kama vile vipasuo kuwa vipasuo kwamizi kupitia uyeyushaji wa irabu. Pia, kipasuo kuwa likwidi au sauti za likwidi kutokana na uimarishaji au udhoofishaji wa konsonanti. Vilevile, uchunguzi ulibaini kuwapo kwa mageuzi si-kamilifu ambayo huhifadhi umbo asilia la mzizi wa neno la MB katika lugha ya Kinyakyusa. Pia kulibainika kuwapo kwa mageuzi kamilifu ya kimofolojia ambayo hayahifadhi umbo asilia la msamiati wa MB katika lugha za Kibantu. Kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika umbo la msamiati pekee, tafiti zingine zijazo zinaweza kuchunguza kuhusu mageuzi na/au uhifadhi wa maana kupitia toni na miundo ya tungo kutoka Mame-Bantu kwenda lugha nyingine za Kibantu, kikiwamo Kiswahili.

**Maneno muhimu:** Mageuzi ya Kimofolojia, Mame-Bantu, Kinyakyusa, Msamiati, Kibantu.

**UTANGULIZI**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mageuzi ya kimofolojia ya maumbo ya vitenzi na nomino kutoka MB kwenda lugha za Kibantu kwa kurejelea mifano ya Kinyakyusa. Mageuzi ya maumbo ya lugha ni mchakato unaopitia vipindi mbalimbali vya kihistoria. Vipindi hivyo vinahusiana na mabadiliko ya kiutamaduni, kijamii, kiutawala pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia (Knowles, 1997; Blythe & Coft, 2021). Sababu hizi huongeza kasi ya mwingiliano baina ya masilugha na kuibua mabadiliko katika kaida za kisarufi na kiisimu kimajumui (Sinnemäki et al., 2024). Katika muktadha wa lugha za Kibantu, mabadiliko haya ya kidayakronia (Bostoen & Guérois, 2022), yamesababisha utofauti mkubwa wa kimofolojia miongoni mwa lugha zenye asili moja, hasa zile za Kibantu. Kwa mujibu wa Sinnemäki na wenzake (2024), utofauti huo unasababishwa na kuongezeka kwa kasi ya mwingiliano huo baina ya wazungumzaji inayounda kaida mpya za kisarufi.

Kihistoria, lugha za Kibantu zilichimbuka takribani miaka 3,500 hadi 5,000 iliyopita kutokea katika eneo la mpaka wa sasa wa Kameruni na Nigeria (Bostoen, Schryver & Pacchiarotti, 2022). Kutokana na hamahama iliyosababishwa na kukua kwa shughuli za kiuchumi na vita, wazungumzaji wa lugha hiyo walihama na kusambaa katika maeneo mengi ya kusini na mashariki mwa Afrika (Batibo, 1987). Kwa kadiri ya maelezo ya Heine na Nurse (2000), msambao huu ulisababisha kuibuka kwa jamii ndogo takribani 5000 za lugha anuwai za Kibantu, kikiwamo Kinyakyusa. Kwa hiyo, kuibuka kwa jamii lugha hizi kunatajwa kusababisha maachano na tofauti za kiisimu, hasa katika kiwango cha matamshi, maana na maumbo ya maneno baina ya lugha za Kibantu na Mame-Bantu (MB). Katika utafiti huu, lugha ya MB inarejelea lugha ya kihenga inayosadikika kuwa msingi wa kihistoria wa lugha zote za Kibantu zilizopo sasa, kikiwamo Kinyakyusa (Bostoen, 2016).

Kadiri ya maelezo ya Van de Velde (2022), lugha ya Kinyakyusa iko katika kundi la M31 kulingana na uanishaji wa Guthrie (1999). Van de Velde (ameshatajwa) anaendelea kueleza kwamba Kinyakyusa ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa na watu wa kabila la Wanyakyusa, ambao hupatikana kusini mwa Tanzania, hasa katika Mkoa wa Mbeya, hususani katika maeneo ya wilaya ya Rungwe na Kyela. Lugha hii ni mojawapo ya lahaja za Kibantu, ikiwa na uhusiano wa karibu na lugha nyingine za eneo hilo kama Kisafwa, Kimbindi na Kinyiha (Robinson, 2016). Kwa mujibu wa maelezo ya Robinson (ameshatajwa), kama ilivyo kwa lugha nyingi za Kibantu, Kinyakyusa kina mfumo wa ngeli za nomino, vitenzi vyenye viambishi vya wakati na nafsi, na mizizi ya maneno inayotokana na mfumo wa kihistoria wa MB.

Ni muhimu kutambua kwamba kiasili, lugha hujitengeneza yenyewe kulingana na mageuzi ya msamiati, matamshi, miundo, muktadha na maumbo kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza maisha ya mwanadamu ambazo pia huzaliwa, hukua na hatimaye kufa (Janda & Joseph, 2003). Chambilecho (2003) anasema mageuzi hayo ya lugha hayawezi kuamuliwa na utashi wa mtu bali muda pamoja na mwachano wa kanuni za kiisimu baina ya lugha zinazohusiana kiisimu. Kutokana na hoja hizo, watafiti wengi wameshughulika na suala la mageuzi ya mofolojia ya lugha ya binadamu katika uwanja wa isimu kwa miongo kadhaa kimajumui. Hata hivyo, McCathy (2010) anaeleza kuwa miongoni mwa mambo ambayo yamechunguzwa zaidi ni uwepo wa sifa fulani za kimofolojia baina ya lugha, mahusiano ya mofolojia na vipengele vingine vya sarufi pamoja na namna vipengele hivyo vinavyosababisha mageuzi ya kimofolojia katika lugha husika.

Kwa mujibu wa Heine na Nurse (2000:3), "mageuzi ya kimofolojia kutoka MB kwenda lugha nyingine za Kibantu yanachagizwa na kuwapo kwa msamiati wa msingi wa MB pasipokuwa na sarufi". Hii inamaanisha kwamba usarufishaji hauna budi kutokea kutokana na utofauti katika idadi ya vitamkwa baina ya MB na lugha nyingine za Kibantu. Wakishadadia hoja hiyo kwa mifano, François (2016) na Harya (2016) wanafafanua kuwa lugha huwa na mageuzi ya ndani ya kimofolojia ambayo mara chache huweza kutoholewa na kutumika katika lugha nyingine zenye asili moja ili kukidhi matakwa ya upekee na utoshelevu wa kisarufi katika lugha husika. Mathalani, katika lugha ya Kilatini ambayo inatajwa kama MB ya Kiingereza cha sasa, kunadhihirika mabadiliko ya maumbo ya maneno kama vile *predicare (hubiri) kwenda predigan/predigen, *templum (hekalu) kwenda tempal/temple na *speculum (kioo) kwenda spiagal/Spiegel (Harya 2016:111). Kwa maelezo ya Harya (ameshatajwa), mageuzi haya kutoka MB (Kilatini) kwenda Kiingereza

cha sasa si ya muda mfupi, bali yanakadiriwa kuanza tangu 1350 hadi 1650 KK. Hamans (2017) anatanabaisha kuwa mageuzi haya ya kimofolojia siyo matokeo ya nguvu wala michakato inayotabirika bali huchagizwa kwa kiasi kikubwa na tabia za watumiaji wa lugha husika kulingana na miktadha ya kimawasiliano.

Halikadhalika, katika muktadha wa lugha za Kibantu, tafiti zinaonesha kuwa mageuzi ya kimofolojia kutoka MB kwenda lugha nyingine za Kibantu ni ya kidayakronia (Idiotov, 2022; Bostoen & Guérois, 2022). Kwa mujibu wa BAKITA (2022), mageuzi ya kidayakronia katika lugha hutokea katika vipindi mbalimbali vya kihistoria miongoni mwa masilugha. Kimsingi, dhana tunayolenga kuifafanua hapa ni kwamba mageuzi ya lugha hayatokei ghafla bali taratibu. Mfano, udondoshaji au uchopekaji wa baadhi ya maumbo katika maneno ya lugha mama mara nyingi huathiri maumbo ya viambajengo vya maneno husika kama vile silabi, mofu au hata neno zima.

Akirejelea lugha za ukanda wa Jukonoidi (Kikutebu na Kibezeni), Kempf (2018) anafafanua kwamba kwa kiasi kikubwa, lugha hizi zinaonekana kutofautiana katika mageuzi ya maumbo kutoka Mame-Niger-Kongo (MNK). Kwa maelezo ya Kempf (ameshatajwa), Kikutebu kinaonekana kuhifadhi maumbo ya MNK ilihali Kibezeni kikishindwa kuhifadhi baadhi ya maumbo ya lugha hiyo. Hii inamaanisha kwamba baadhi ya lugha za Kibantu, kikiwamo Kinyakyusa, zinaweza kuhifadhi maumbo ya MB kiasi cha kutokuwapo kwa mageuzi makubwa yanayoweza kuathiri ama matamshi, maana au mpangilio wa viambajengo katika neno husika. Licha ya ufafanuzi uliopo kuhusu mageuzi ya maumbo ya maneno kutoka MB kwenda lugha nyingine zinazohusiana, haijafahamika kwa uwazi namna mageuzi haya yanavyodhihirika kutoka MB kwenda Kinyakyusa.

Tafiti nyingi zilizopo zimejikita katika kuchunguza mageuzi ya viambishi na maumbo ya maneno kwenye lugha za Kibantu za Ukanda wa Kati na Magharibi, huku zikibainisha jinsi usarufishaji unavyoweza kudondosha au kubadilisha maumbo ya MB (Bostoen, 2016). Mienendo hii ya mageuzi ya maumbo bado haijafafanuliwa kwa uwazi katika lugha za Kibantu za Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Tanzania, hususani Kinyakyusa. Tafiti za kijumla za kiisimu za Heine (2012), François (2016), Harya (2016), Hamans (2017), na Bostoen na Guérois (2022) zinadokeza tu sheria za jumla za mabadiliko ya lugha mbalimbali kimajumui bila kuonesha kipekee jinsi maumbo ya msingi ya MB yanavyohifadhiwa au kugeuzwa katika Kinyakyusa. Kwa hiyo, kulikuwa na haja ya kuchunguza mageuzi ya maumbo ya msamiati wa msingi, hususani vitenzi na nomino za MB kwenda katika lugha ya Kinyakyusa ili kuelewa ikiwa Kinyakyusa kimehifadhi au kudondosha maumbo asilia ya MB.

**Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia (NMA) iliyoasisiwa na Wolfgang U. Dressler kwa kushirikiana na Willi Mayerthaler, Oswald Panagl, na Wolfgang U. Wurzel katika kazi yao ya mwaka 1987. Kwa mujibu wa Dressler na Kilani-Schoch (2016), NMA ni nadharia ya kiuamilifu na kisaikolojia inayojikita katika kudhania kuwa mifumo ya kimaumbo katika lugha za binadamu ina mienendo inayofuata kanuni asilia za kiisimu na kiakili. Kanuni hizi hutumiwa na masilugha, aghalabu, kurahisisha mchakato wa upokeaji na uzalishaji wa matamshi, maumbo na maana za maneno. Katika muktadha wa kidayakronia, nadharia hii inatazama mageuzi ya lugha kama mchakato ambapo mifumo ya kimaumbo huacha hali ya ugumu na kuelekea kwenye hali ya uasili au wepesi wa kiutambuzi. NMA inasimamiwa na vigezo vikuu vitatu vya upendeleo wa kiasili ambavyo vinatoa dira ya kupima kiwango cha mageuzi au uhifadhi wa maumbo kutoka MB kwenda lugha nyingine.

Kwanza, kanuni ya uhusiano wa uwili-pacha wa kipekee. Kanuni hii inaeleza kuwa umbo asilia zaidi ni lile linaloonesha uhusiano wa moja kwa moja baina ya maana na umbo la neno. Katika dhana ya uwili-pacha, kanuni hii inaeleza kuwa uhusiano bora ni ule ambapo mofu moja inawakilisha dhana moja pekee ya kisarufi. Utafiti huu ulitumia kigezo hiki kuchunguza ikiwa mageuzi kutoka MB yanasababisha Kinyakyusa kudumisha upekee wake au kupoteza upekee huo kupitia hali ya mofu moja kubeba maumbo mengi.

Pili, ni kanuni ya upenyezi au uwazi wa kiumbo. Upenyezi huu unahusisha urahisi wa mtumiaji wa lugha kubaini mipaka kati ya mofu mbalimbali zilizounda neno bila kuwepo kwa mabadiliko ya kifonolojia yanayofifisha umbo la mizizi au viambishi vya neno. Kanuni hii inaeleza kuwa umbo asilia la neno linadhihirika ikiwa mizizi na viambishi vyake

vimetenganishwa kwa uwazi. Dressler (1987) anafafanua kuwa mara nyingi, mabadiliko ya lugha kidayakronia huathiri upenyezi huu kupitia michakato ya kimofofonolojia. Kigezo hiki kilitusaidia kubaini jinsi Kinyakyusa kilivyorekebisha maumbo ya vitenzi na nomino za MB ili kurahisisha utambuzi na matamshi yake kwa wazungumzaji.

Tatu, ulinganifu wa kimfumo: kigezo hiki kinashughulikia jinsi umbo maalumu linavyoendana na muundo asilia wa lugha husika. Kanuni hii inaeleza kwamba mageuzi ya maumbo ya maneno hayatokei kiholela; badala yake, lazima yafuate kanuni na mifumo ya ndani ya kisarufi inayokubalika katika lugha husika. Katika utafiti huu, kigezo hiki kilitusaidia kufafanua namna maumbo ya MB yanavyofungamana na kuhifadhiwa katika Kinyakyusa.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kitaamuli, yaani maelezo, katika kubainisha mageuzi ya maumbo ya maneno pamoja na kufafanua michakato inayohusika katika mageuzi ya maumbo husika kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa. Kijiografia, utafiti huu ulifanyikia Wilaya ya Rungwe iliyoko Mkoa wa Mbeya. Eneo hili liliteuliwa kwa makusudi kwa kuwa ndilo chimbuko kuu la kijiografia na kiutamaduni la wazungumzaji asilia wa lugha ya Kinyakyusa nchini Tanzania (Maho, 2009; Muzale & Rugemalira, 2008). Kwa hiyo, lilimwezesha mtafiti kupata watafitiwa wenye uelewa, tajiriba na ujuzi wa lugha ya Kinyakyusa ambao walitumika kufasiri maumbo ya maneno ya MB yaliyochambuliwa maktabani.

Mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji lengwa wa kipekee kuteua sampuli ya matini ya Bostoen (2009) yenye msamiati wa MB pamoja na watafitiwa watano (05) ambao ni wazungumzaji asilia wa Kinyakyusa. Kupitia matini hiyo, jumla ya maumbo 25 ya nomino na 10 ya vitenzi ya msamiati wa msingi wa MB yaliteuliwa kwa makusudi. Maumbo haya yalizingatiwa kuwa kielelezo tosha kwa kuwa yanabeba dhana za msingi zisizobadilika kirahisi kama vile viungo vya mwili, viumbe hai na matendo ya msingi ya kibinadamu. Hata hivyo, ili kuthibiti ubora wa data zilizochambuliwa kutoka kwenye matini ya Bostoen (ameshatajwa), watafitiwa sita (06) waliteuliwa miongoni mwa wazungumzaji asilia wa Kinyakyusa wilayani Rungwe. Idadi hiyo ya watafitiwa ilitosheleza kwa sababu utafiti wa kitaamuli unahitaji utoshelevu wa data. Vigezo maalumu vilivyotumika kuwateua watafitiwa hao ni umri, jinsia na umahiri wa lugha, ambapo utafiti ulihusisha wazungumzaji wa Kinyakyusa wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 60. Kigezo hiki kilitumika kwa sababu kundi hili kwa kawaida lina uwezo wa kufahamu maumbo na mabadiliko yake kwa namna wanavyoitumia lugha kwa kipindi kirefu. Katika kigezo cha jinsia, mtafiti aliteua watafitiwa wa kike watatu (03) na wa kiume watatu (03) ili kupata uwakilishi mpana wa kijinsia. Fauka ya hayo, watafitiwa wote waliombwa ridhaa ya kushiriki katika utafiti na kuhakikishiwa usiri wa taarifa zao.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia njia za uchambuzi matini na usaili. Uchambuzi matini ulitumika kuchambua matini ya msamiati wa msingi wa Mame-Bantu ya Bostoen (2009). Njia hii ilisaidia kubainisha maumbo 25 ya nomino na 10 ya vitenzi vya msamiati wa msingi wa MB. Aidha, njia ya usaili ilitumika kuwasaili wazungumzaji asilia wa Kinyakyusa kwa lengo la kupata tafsiri ya maumbo ya maneno husika katika Kinyakyusa. Kupitia mbinu ya usaili huria, watafitiwa waliombwa kutoa visawe halisi vya Kinyakyusa vinavyoendana na dhana za maumbo ya msamiati wa MB yaliyoteuliwa. Usaili huu ulirekodiwa kwa simu na kunakiliwa katika maandishi. Kwa hiyo, data zilizotokana na usaili huu ziliwezesha kubaini mageuzi ya maumbo ya maneno yaliyofanyika kutoka MB kwenda Kinyakyusa.

Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Usimbishaji huu ulifanyika kwa kuzingatia hatua sita. Kwanza, mtafiti alisoma matini teule na kusikiliza rekodi za sauti kwa kurudiarudia ili kubaini maudhui yanayohusiana na majibu yaliyotarajiwa. Pili, aliunda misimbo maalumu kulingana na mwelekeo wa data zilizokusanywa kisha kuihusianisha na mageuzi ya maumbo yaliyobainika kutoka MB kwenda Kinyakyusa. Tatu, alilinganisha maumbo ya maneno teule ya MB na yale ya Kinyakyusa. Nne, alilinganisha matamshi ya maumbo ya maneno husika ili kubaini mabadiliko ya vitamkwa yanayodhihirika kutoka MB kwenda Kinyakyusa. Tano, alibainisha aina ya mageuzi (kamilifu na/au si kamilifu) ya maumbo ya maneno yaliyochunguzwa na kufafanua michakato ya kiisimu inayohusika katika mageuzi hayo. Mwisho, alifafanua kuwapo au kutokuwapo kwa

mageuzi ya maumbo yanayoweza kusababisha neno kuhifadhi umbo asilia, hasa vitamkwa vinavyounda mzizi, au kupoteza kabisa sifa ya upekee wa uwili pacha baina ya umbo la neno na maana yake.

## MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti uliozaa makala hii ulibaini kuwapo kwa mageuzi ya mofolojia ya nomino na vitenzi kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa. Mageuzi haya yanasababishwa na ufanyikaji wa michakato mbalimbali ya kimofofonolojia kama vile uyeyushaji wa irabu, usilimishaji wa konsonanti, uchopekaji, udondoshaji, ulikwidishaji pamoja na ukaakaishaji. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kuwa mageuzi haya yanaathiri hifadhi ya maumbo asilia ya msamiati wa msingi wa MB katika Kinayakyusa.

Hii ni kutokana na kuwapo kwa ongezeko la vitamkwa na maumbo mapya ya msamiati katika lugha ya Kinyakyusa. Hivyo, utafiti uliofanyika umebaini kuwa kati ya mauombo 35 yaliyochunguzwa, maumbo saba ya nomino na mawili (02) yalionesha mageuzi kamilifu ya kiumbo, huku maumbo 26 yakiwa na mageuzi yasiyo kamilifu, yaani licha ya kuwapo kwa mageuzi makubwa ya vitamkwa, bado yanahifadhi umbo asilia la mzizi wa neno la MB katika Kinyakyusa.

### Mageuzi ya Maumbo ya Nomino kutoka MB kwenda Kinyakyusa

Lugha ya Mamebantu ina msamiati wa msingi ambao unajumuisha makundi mbalimbali ya nomino. Makundi hayo ya nomino yanatokana na shughuli mbalimbli za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni pamoja na kimazingira ambazo zilikuwa zikifanywa na watu wa jamii ya lugha za Kibantu (Christopher, 1967; Palome, 1975). Matokeo yanaonesha kuwapo kwa mageuzi ya kimofolojia katika nomino zinazotaja viungo vya mwili pamoja na nomino zinazotaja tarakimu za chini, yaani moja hadi sita.

### Mageuzi ya Maumbo ya Nomino Zinazotaja Viungo vya Mwili

Haya ni mabadiliko yanayojitokeza katika nomino zinazotaja viungo vya mwili kama vile mdomo, mkono, sikio, jicho ndevu na ulimi. Data zinaonesha kwamba maumbo ya nomino hizo yamebadilika kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa. Mabadiliko hayo ni kuongezeka kwa idadi ya mofu zinazounda nomino hizo au ubadalalishaji wa umbo zima la nomino. Jedwali Na. (1) linaonesha mabadiliko hayo.

**Jedwali Na. 1: Mageuzi ya Maumbo ya Nomino Zinazotaja Viungo vya Mwili kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

| Na. | Mame-Bantu | Kinyakyusa | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | *book | iki-b(h)oko | mkono |
| 2 | *(le) – iso / jico | il-iso | jicho |
| 3 | *(ku) – toi | imbulu-kutu | sikio |
| 4 | *(mu) – nywa /domo | un-domo | mdomo |
| 5 | *da | palua-da | tumbo |
| 6 | *i-jíno | il-ino | jino |
| 7 | *mʊ-kíla | imbikipiki | mkia |
| 8 | *dèdù | in-defu | ndevu |
| 9 | *dɪmè | ulu-limi | ulimi |

Data za Uwandani (2025)

Jedwali Na. (1) linaonesha kuwapo kwa mageuzi ya maumbo ya nomino zinazotaja viungo vya mwili kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa. Katika jedwali hili tunaona kwamba maumbo ya umoja iki-, il-, imbulu, un-, palua-, in- na ulu- yanadhihirika katika Kinyakyusa ilihali maumbo hayo hayakuwepo katika Mame-bantu. Kwa hiyo, kuna ongezeko la maumbo ambayo hayapo katika nomino za Mame-Bantu. Vilevile, tunabaini kuwapo kwa umbo jipya la *imbikipiki* (mkia) linalotofautina kabisa na neno la Mame-Bantu.

Kwa mujibu wa Nurse (1983), mabadiliko haya yanasababishwa na kuwapo kwa utofauti wa vitamkwa pamoja na mwachano wa kijiografia baina ya

lugha za jamii ya Kibantu. Hii inamanisha kuwa, kihistoria Mame-bantu ilikuwa na vitamkwa (fonimu) vichache ambavyo vinatumika kama msingi wa kuzalisha vitamkwa vingi vyenye asili ya sehemu moja ya utamkaji na kutofautiana katika namna ya utamkaji. Mfano, kuna mageuzi ya kipasuo cha ufizi /d/ kwenda kimadende /r/ au kitambaza /l/ kama ilivyo katika *dɪmè - limi, kipasuo cha mdomo /b/ kwenda kikwamizi cha mdomo /bh/ mfano katika *boko – b(h)oko[2], mabadiliko ya mfuatano wa fungu irabu /oi/ kwenda /u/ katika *ku-toi – kutu, pamoja na mabadiliko ya /d/ kwenda /nd/ katika *dèdù - ndefu katika Kinyakyusa. Kuhusu umbo la nomino b(h)oko, ni muhimu tukaweka bayana kwamba, katika rejea za Kinyakyusa zilizopo kama vile Biblia (*Ibangili*) na nyimbo katika kitabu cha *Mwamba* na kile cha *Inimbo sya Kilisiti* "iki-boko" ndilo hutumika japokua katika matamshi wazungumzaji hutumia kikwamizi cha mdomo /bh/ ambapo hutamkwa kwa kuziba hewa na kuruhusu itoke taratibu kama ulivyoweka hapo /bh/. Kwa hiyo, tulijumuisha /bh/ kama badiliko katika nomino husika kwa sababu linadhihirika katika matamshi ya wazungumzaji asilia wa Kinyakyusa.

**Mageuzi ya Maumbo ya Nomino Zinazotaja Tarakimu za Chini (1 hadi 6)**

Haya ni mabadiliko yanayohusu nomino zinazotaja tarakimu za chini kama vile moja, mbili, tatu, nne, tano jna sita. Nomino za Mame-bantu zinazotaja tarakimu za kuanzia moja hadi tisa hazina mageuzi ya kidhana, bali ongezeko la mofu katika mzizi wa neno, mabadiliko ya baadhi ya vitamkwa katika neno pamoja na uzalishaji wa maumbo mapya yasiyokuwepo katika Mame-Bantu. Mageuzi haya yanayaosababishwa na utofauti katika utamkaji wa baadhi wa sauti za Mame-bantu katika lugha mbalimbali za Kibantu kikiwamo Kinyakyusa (Pozdniakov, 2018). Jedwali Na. (2) linaonesha mageuzi hayo:

**Jedwali Na. 2: Mageuzi ya ya Maumbo ya Nomino Zinazotaja Tarakimu za Chini (1 hadi 6) kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

| Na. | Mame-Bantu | Kinyakyusa | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | *moi | ka-mu | 1 (moja) |
| 2 | *bidi | tu-bhili | 2 (mbili) |
| 3 | *tato | tu-tatu | 3 (tatu) |
| 4 | *ne | tu-na | 4 (nne) |
| 5 | *tááno/ʊ́ | ntandatu | 5 (tano) |
| 6 | *tʊ́ʊ́bá | peteli | 6 (sita) |

Data za Uwandani (2025)

Jedwali Na. (2) linaonesha kuwapo kwa ongezeko la mofu za umoja na wingi katika nomino zinazotaja tarakimu kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa ambapo; maumbo mapya ya *ka-*, *tu-*, *ntandatu* pamoja na *peteli* yanatumika katika kudokeza dhana ya idadi inayobebwa na nomino za tarakimu 1, 2, 5 na 6 kwa mtawalia. Pia, tunabaini kuwapo kwa mabadiliko ya ubadalalishaji wa irabu kutoka /oi/ kwenda /u/ (*moi – kamu), /b/ kwenda /bh/ na /d/ kwenda /l/ (*bidi- bhili), /o/ kwenda /u/ (*tato-tatu), /e/ kwenda /a/ (*ne -na). Vilevile kuna mabadiliko ya ubadalalishaji wa umbo zima la neno kama ilivyo katika *tááno/ʊ́ – ntandatu* pamoja na *tʊ́ʊ́bá – peteli. Kwa mujibu wa Pozdniakov (2018), mageuzi hayo yanasababishwa na mchakato wa kimofofonolojia, ambapo baadhi ya matamshi ya vitamkwa hubadilika kutokana na ama muunganiko au mwachano wa sauti fulani katika lugha hususani wakati wa utamkaji wa maneno hayo. Hata hivyo, maumbo hayo hayadhihiriki katika Mame-bantu suala linalotufanya tudhani kuwapo kwa mageuzi ya kimofolojia katika mofu za nomino husika.

**Mageuzi ya Maumbo katika Nomino Zinazotaja Mazingira kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

Haya ni mabadiliko yanayohusu majina yanayotaja hali ya hewa, shughuli za kawaida za kijamii, uoto wa asili pamoja na vitu asilia vilivyowazunguka watumia lugha kama vile maji, milima, mawe, mchanga, udongo, upepo, miti pamoja na majira ya mwaka (Palome, 1975). Hivyo, lugha za Kibantu kikiwamo Kinyakyusa zimeiga baadhi ya maumbo ya nomino hizo ingawa, kuna mageuzi yanayojichomoza katika baadhi ya maumbo ya maneno husika kama inavyoonekana katika jedwali Na. (3):

**Jedwali Na. 3: Mageuzi ya Maumbo katika Nomino za Zinazotaja Mazingira kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

| Na. | Mame-Bantu | Kinyakyusa | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | *nyàmà | i-nyama | nyama |
| 2 | *njɪla | u-sebho | njia |
| 3 | *kʊ̀ʊ̀gʊ | il-yubha | muwa |
| 4 | *kádà | u-nkala | mkaa |
| 5 | *jʊ̀nì | in-juni | ndege |
| 6 | *bʊ́à | i-mbwa | mbwa |
| 7 | *pépò | m-bepo | upepo |
| 8 | *tɪ́ | m-piki | mti |
| 9 | *bʊ̀è | ii-bhwe | jiwe |
| 10 | *jíjɪ̀ | a-misi | maji |

Data za Uwandani (2025)

Tukichunguza data kutoka katika Jedwali Na. (3), tunabaini kuwapo kwa mageuzi ya maumbo ya nomino kutoka Mamebantu kwenya Kinyakyusa. Mabadiliko hayo ni kuongezeka kwa viambishi awali vya umoja na wingi {i-}, {u-}, {il-}, {in-}, {m-}, {ii-} pamoja na {a-}; ambavyo vinadokeza umoja wa nomino husika katika Kinyakyusa ilihali havipo katika Mame-bantu. Vilevile, kuna mageuzi ya baadhi ya fonimu kama vile; /k/ kwenda /nk/ (*kádà-nkala), /j/ kwenda /nj/ (*jʊ̀nì - njuni), /p/ kwenda /mb/ (*pépò -mbepo), /b/ kwenda /bh/ (*bʊ̀è - iibhwe), /ue/ kwenda /w/ (*bʊ̀è- i-bhwe, *bʊ́à - imbwa). Pia kuna mageuzi yanayohusisha umbo zima la nomino kama ilivyo katika *njɪla –usebho, *kʊ̀ʊ̀gʊ - ilyubha, *tɪ́ – mpiki pamoja na *jíjɪ̀ – amisi. Nurse (1983) anaeleza kuwa, mageuzi ya vitamkwa yanayodhihirika katika Kinyakyusa yanasababishwa na michakato mbalimbali ya kimofofonolojia kama vile uyeyushaji na usilimishaji irabu na konsonanti mtawalia.

Uyeyushaji ni mchakato wa kimofofonolojia unaohusisha mageuzi ya sauti za irabu juu /u/ kuwa kiyeyusho /w/ au /i/ kuwa /y/ katika mazingira ya kufuatiwa na irabu nyingine isipokuwa zenyewe (Mndeme & Ligembe, 2022; Mukanda 2022). Kwa mujibu wa Mndeme (ameshatajwa), mchakato huu hauathiri umbo la neno pale pale zisizofanana /u/ na /i/ zikifutiwa na irabu nyingine zote isipokuwa zenyewe kama ilivyo katika *bʊ̀è- i-bhwe na *bʊ́à – imbwa. Kuhusu usilimishaji wa konsonanti, Siame & Wenzake (2024) wanafafanua kwamba, huu ni mchakatao unaohusisha mageuzi ya sauti zisizo za ung'ong'o kuwa na sifa ya ung'ong'o katika mazingira ya sauti husika kutanguliwa na sauti ya ung'ong'o, mfano *kádà-nkala, *jʊ̀nì – njuni, *bʊ́à - imbwa. Katika mifano hii, tunaona king'ong'o cha ufizi /n/ kikifuatiwa na kipasuo cha kaakaa laini /k/ hubadilika na kutamkwa kama sauti moja ya ung'ong'o /nk/. Vivyo hivyo, king'ong'o cha mdomo /m/ kinapofuatiwa na kipasuo cha mdomo /b/ hubadilika na kutamkwa /mb/. Kimsingi, haya ni mabadiliko makubwa katika umbo la kitenzi cha Mame-Bantu kwa sababu kiasili lugha hii haina sauti za namna hii (Nurse, 1983). Ni muhimu kutambua kwamba, mageuzi haya hayatokei kiholela tu, bali kwa kuzingatia kanuni mahususi zinazofanya kazi katika mazingira maalumu ya mfuatano wa vitamkwa katika neno.

Hata hivyo, tafiti zinaonesha kuwa siyo mara zote mageuzi ya vitamkwa katika neno yanaweza kutokea kwa sababu ya mchakato wa kimofofonolojia bali, mazingira au umbali wa kijiografia kutoka jamii lugha moja kwenda nyingine (Hyung-Soo, 1999; Kula & Kadenga, 2015). Kwa mujibu wa Hyung-Soo (Ktj), miongoni mwa vipengele vinavyoweza kusababisha utofauti baina ya lugha ni ufanyikaji wa michakato ya kimofolojia. Anaendelea kueleza kuwa, licha ya michakato hiyo kuwa ya kimajumui, lakini kuna baadhi ya mazingira yanayoonekana kutofautiana kutoka lugha za eneo moja hadi lingine ama zenye asili moja au tofauti kama ilivyo Kiswahili na Kinyakyusa dhidi ya Kikorea. Akishadadia hoja hiyo, kwa kubainsha tofauti za kimatamshi kati ya lugha za Kizulu Kiyeyi na Kixhosa, zinazozungumzwa kusini mwa Afrika, Maddieson (2019:1) anasema: ijapokuwa lugha nyingi za Kibantu zina fonetiki sawia, kuna tofauti

ndogondogo za kifonolojia kutoka lugha moja na nyingine. Baadhi ya tofauti hizi zinaweza kusababishwa na mtawanyo wa kimatamshi na kiothografia, ambao pia unaweza kurekebisha tofauti baina ya lugha husika.

Hii ina maana kwamba licha ya kuwapo kwa mfanano hususani wa nduni za kiprosodiki katika matamshi ya sauti baina ya lugha husika, mwachano wa kijiografia baina ya lugha hizo unasababisha kuwapo kwa tofauti kutoka lugha moja na nyingine. Kwa mfano, lugha za Kaskazini-Magharibi, katika eneo la Pwani ya Mashariki na Kusini-Mashariki mwa Afrika ya Kusini (Kizulu na Kikhosa), angalau zina vipasuo vya mdomo, ambacho hakipo katika jamii lugha za Kibantu za Bonde la Kongo na Kusini Magharibi mwa Afrika ya Kusini (Maddieson, Ktj). Anaendelea kufafanua kwamba, vipasuo kwamizi pia, vinadhihirka kwa utofauti miongoni mwa lugha za Kibantu za Afrika ya Kusini ingawa, wakati mwingine zinatokea kama alomofu za vipasuo sighuni katika baadhi ya lugha za Afrika ya Kusini na Afrika ya Mashariki; ambazo baadhi zinasadikika kutohoa matamshi kutoka lugha za kundi la Afro-Asia yaani, Kikushi (Maddieson, Ladefoged & Sands 1999). Kimsingi, dhana tunayolenga kuilezea hapa ni kwamba utofauti katika utamkaji wa sauti kutoka kwa makundi ya jamii lugha moja yanayoachana kijiografia, unaweza kusababisha mageuzi ya maumbo ya sauti na hatimaye mofolojia ya nomino baina ya lugha hizo.

Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha mwelekeo wa kipekee wa lugha ya Kinyakyusa katika kuhifadhi na kugeuza maumbo ya MB. Kwa maana nyingine, licha ya Meeussen (1967) kubainisha kuhusu ujenzi upya wa MB kwa kuonesha viambishi awali rahisi kama vile **mʊ-* au **kɩ-*, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kuwa Kinyakyusa kimeongeza viambishi awali vya ziada kama unavyoonekana katika mofu {iki-} katika iki-b(h)oko (mkono), {il-} katika il-iso (jicho), na {ulu-} kaatika ulu-limi {ulimi}. Hali hii inaendana na maelezo ya Van de Velde (2019) yanayobainisha kuwa lugha ya Kinyakyusa ina mifumo thabiti ya viambishi awali inayotumika kuimarisha utambulisho wa ngeli na dhima ya urejeleaji. Hata hivyo, Nurse (2008) anabainisha kwamba mchakato huu wa kuongeza mofu unaweza kutazamwa kama mkakati wa kimofolojia wa kuimarisha mfumo wa ngeli ili kurahisisha upatanishi wa kisarufi katika sentensi za lugha husika. Fauka ya hayo, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mageuzi ya kimofolojia, aghalabu, huchagizwa na mabadiliko ya vitamkwa. Mathalani, nomino kama *il-iso* (jicho) na *il-ino* (jino) zinathibitisha uhifadhi wa sauti ya kitambaza /l/ ambayo ni inaakisi mabadiliko ya kipasuo cha ufizi */d/ cha MB, hasa baada ya sauti hiyo kuimarishwa kupitia mchakato wa ulikwidishaji.

Halikadhalika, japokuwa tafiti nyingi za kidayakronia kueleza kuwa konsonanti ya awali **j*, kama ilivyo katika **jícò* na **jínò*, ilipotea au kuungana na irabu katika lugha nyingi za Kibantu (Wills, 2022), Kinyakyusa kimebakiza umbo hilo la MB. Kwa kurejelea kanuni ya upenyezi na uangavu wa kiumbo, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kuwa Kinyakyusa kimeweza kudumisha mpaka wa wazi kati ya kiambishi na mzizi wa neno. Hali hii inathibitisha kuwa Kinyakyusa ni lugha hafidhina inayohifadhi misingi ya kihenga, huku ikifanya marekebisho madogo ya kifonolojia yasiyoweza kuathiri umbo na maana ya neno.

Licha ya ukweli kwamba msamiati wa msingi kama viungo vya mwili huchukuliwa kuwa mgumu kubadilika, matokeo ya utafiti yanabaini kuibuka kwa umbo jipya kabisa katika baadhi ya nomino, mfano, *imbikipiki* (mkia) badala ya **mʊ-kíla*, *m-piki* (mti) na *u-sebho* (njia). Mabadiliko haya yanashabihiana na hoja za Bostoen na Bastin (2016) kuwa ujenzi upya wa msamiati unapaswa kuzingatia mabadiliko ya ndani yanayosukumwa na mwingiliano wa kijamii na mahitaji ya wasemaji. Hata hivyo, kupitia kanuni ya uwili-pacha ya NMA, mageuzi haya ya umbo zima yanaweza kutazamwa kama jitihada ya lugha kuelekea kwenye upekee wake, ambapo mzungumzaji anaunda alama ya kipekee kwa ajili ya dhana mahususi ili kuondoa utata na kurahisisha mchakato wa kiakili wa utambuzi wa lugha (Dressler & Kilani-Schoch, 2017).

Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa mageuzi ya kimofolojia katika Kinyakyusa yanafuata kanuni asilia zinazolenga kurahisisha upokeaji na uzalishaji wa lugha. Licha ya kuwapo kwa michakato kama udondoshaji wa vitamkwa, Kinyakyusa kimefanikiwa kudumisha upekee na uangavu wa maumbo kulingana na muundo wake wa asili ambao unatajwa na Dressler (1987) kama msingi mkuu wa mofolojia asilia katika kueleza mageuzi ya kidayakronia ya lugha za Kibantu.

**Mageuzi ya Maumbo ya Vitenzi kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

Haya ni mabadiliko yanayohusu mabadiliko ya kifonolojia, kimaumbo na kisintaksia yaliyotokea katika historia ya lugha. Baadhi ya vitenzi vilivyokuwa na maumbo tata katika Mame-Bantu yalirahisishwa kwa kupoteza viambishi au kubadilisha mpangilio wa silabi katika Kinyakyusa. Mageuzi haya yanaonesha uendelezaji wa lugha na uhusiano wa kihistoria kati ya lugha za Kibantu (Nurse, 1983; Creissels, 2009). Kwa mujibu wa Nurse (Ktj), aghalabu lugha zote za Kibantu zimesheni miundo na maumbo mbalimbali ya kitenzi cha Mame-Bantu ingawa, kuna baadhi ya vitenzi vinabadili maumbo yake tofauti na yanavyodhihirika katika Mamebantu. Jedwali Na. (4) linaonesha namna mageuzi hayo yanavyodhirika katika lugha ya Kinyakyusa:

**Jedwali Na. 4: Mageuzi ya Maumbo ya Kitenzi kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa**

| Na. | Mame-Bantu | Kinyakyusa | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | *jìj | ugwe-isa | njoo |
| 2 | *fa | fu-la | kufa |
| 3 | *dáad | lambalala | lala |
| 4 | *Cèka | seka | cheka |
| 5 | *dɪ̀d | lila | lia |
| 6 | *kʊ̀d | lusa | vuta |
| 7 | *jɪ̀mb | imba | imba |
| 8 | *pa | -pa | pa |
| 9 | *gàmb | jobha | ongea |
| 10 | *jìkad | tu-g(h)ala | kaa/keti |

Data za Uwandani (2025)

Jedwali Na. (4) linaonesha kuwapo kwa mageuzi ya kimofolojia kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa. Mageuzi hayo yanasababisha kuwapo kwa mambo makuu mawili katika umbo la kitenzu cha Kinyakyusa. Mosi ni mageuzi ya kifonolojia yanayohusisha muhamo wa pahala pa matamshi katika baadhi ya sauti mfano, kutoka kipasuo kwamizi cha kaakaa gumu sighuni /ʧ/ kwenda kipasuo kwamizi cha ufizi sighuni /s/ kama ilivyo katika **cèka –seka.* Pia, kuna mageuzi ya kipasuo cha ufizi ghuni /d/ kwenda kitambaza /l/ yaani ulikwidishaji, mfano katika **dɪ̀d- lila.* Aidha, kuna udondoshaji wa kipasuo kwamizi cha kaakaa gumu /j/ katika mazingira ya kufuatiwa na irabu juu mbele /i/ kama ilivyo katika **jɪ̀mb-imba.* Vilevile, kunadhihirika uchopekaji wa mofu {m-} mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi cha Mame-Bantu katika Kinyakyusa **pa- /m-pa* pamoja na ubadalalishai wa sauti ya kipasuo cha kaakaa laini /k/ na kutamkwa kama kipasuo kwamizi cha kaakaa laini ghuni /gh/. Mabadiliko haya yanadhihirika katika kitenzi **jìkad -tu-ghala.* Mageuzi hayo ya maumbo yanasababishwa na utofauti katika utamkaji wa baadhi ya sauti ambazo kiasili haziko katika Mame-Bantu (Van de Velde, 2022). Hivyo, sauti hizo zinapobadilika zinasababisha pia kugeuzwa kwa umbo zima la Kitenzi cha Kinyakyusa.

Licha ya kuwapo kwa mageuzi yanayochagizwa na matamshi ya baadhi ya sauti, pia kunadhihirika mageuzi ya umbo zima la kitenzi cha Kinyakyusa kisichofanana kabisa na kitenzi cha Mamebantu. Kwa mujibu wa Christopher, (1967) na Guthrie (1948), mageuzi haya hayapangwi na wazungumzaji lugha, bali hutokea kinasibu miongoni mwa lugha nyingi za Kibantu. Kwa mujibu wa Palome (1975), unasibu huu hudhihirika kwa kuwapo kwa utofauti wa maumbo husika kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine kulingana na mwachano wa kijiografia baina ya wazunguzaji wa lugha za Kibantu. Ijapokuwa kuna utofauti baina ya lugha za Kibantu, kwa kiasi kikubwa maumbo ya msamiati wa MB, bado yanaonekana kuhifadhika katika lugha mbalimbali za Kibantu kikiwamo Kinyakyusa.

Kimsingi, matokeo ya utafiti uliofanyika yanadhihirisha michakato tata ya kimofofonolojia ya Kinyakyusa na inayoshabihiana na lugha nyingine za Kibantu, huku ikibainisha sifa zake za kipekee. Licha ya ujenzi mpya

wa MB kuonesha mizizi ya vitenzi ikiwa na muundo rahisi wa konsonanti + Irabu + konsonanti [KIK] (Meeussen, 1967), Kinyakyusa kimeonesha mwelekeo wa kurefusha au kurekebisha maumbo hayo ili kukidhi mahitaji ya mpangilio asilia wa vitamkwa katika maneno ya lugha husika. Kwa mfano, mageuzi ya **cèka* kwenda *seka* (cheka) na **dɪ̀d* kwenda *lila* (lia) yanashabihiana na maelezo ya Philippson (2022) na Maddieson (2003) kuwa konsonanti za **c* na **d* mara nyingi, hupitia mchakato wa ukaakaishaji au ulikwidishaji, mtawalia, katika lugha nyingi za Kibantu, kikiwamo Kinyakyusa. Kwa tafakuri ya kiutafiti, hali hii inalenga kuimarisha utambuzi wa neno kulingana na mfumo wa sauti wa lugha husika.

Kwa upande mwingine, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwapo kwa udondoshaji wa vitamkwa, mfano katika kitenzi **jɪ̀mb* (imba) kinageuzwa na kuwa *imba* katika Kinyakyusa. Mageuzi haya yanatoa ushahidi muhimu katika mjadala wa kidayakronia kuhusu asili ya konsonanti **j*, yaani ni kiyeyusho /y/. Hata hivyo, Wills (2022) anasisitiza kuwa kiyeyusho hiki kinapaswa kurejeshwa kama **(y)ɪ̀mb* au ule wenye kuanza na irabu moja kwa moja, kwani lugha nyingi binti (ikiwemo Kinyakyusa) hazioneshi alama yoyote ya konsonanti ya **j* katika mazingira husika. Japokuwa ujenzi wa Meeussen (1967) unakibainisha kiyeyusho **j* kama kianzio cha msingi, matokeo ya utafiti huu yanaunga mkono madai ya Wills kuwa Kinyakyusa kimehifadhi hali ya asili ya kuanza na irabu, au kudondosha kitamkwa hicho ili kurahisisha matamshi.

Vilevile, kuwapo kwa maumbo kama *lambalala* (lala) badala ya **dáad* na *tu-ghala* (kaa) badala ya **jìkad* kunaashiria mchakato wa urefushaji wa maumbo ya vitenzi. Ijapokuwa ujenzi upya wa maumbo ya MB unaonesha mizizi mifupi, utafiti uliofanyika unaonesha kuwa Kinyakyusa kinafuata kanuni ya uzito wa neno au kigezo cha urefushaji wa kitenzi ili kuongeza uangavu na upekee wa umbo la kitenzi husika. Hali hii inaendana na hoja za Hyman (2018), Bostoen na Guérois (2022) kuwa baadhi ya lugha za Kibantu hupendelea kutumia mfululizo wa viambishi ili kuimarisha dhima ya neno. Licha ya mchakato huu kuonekana kufanya umbo la neno kuwa refu zaidi, Dressler (2003), anaeleza kuwa urefushaji huu unaweza kutazamwa kama jitihada ya kuleta ulinganifu wa mfumo baina ya MB na lugha nyingine za Kibantu, ambapo vitenzi vyote lazima vizingatie muundo mahususi wa silabi na upatanishi wa kisarufi.

Halikadhalika, uvumbuzi wa umbo jipya la *jobha* (ongea) badala ya **gàmb* pia unadhihirisha mageuzi makubwa ya msamiati. Hata hivyo, Devos na Bernander (2022) na Persohn (2017) wanabainisha kuwa Kinyakyusa mara nyingi hutumia vitenzi ambavyo asili yake ni kidayakronia tofauti na ujenzi wa jumla wa MB, pengine, ni kutokana na mwingiliano na maachano ya kijiografia katika Ukanda wa Nyasa-Tanganyika. Ijapokuwa unasibu unatajwa na Guthrie (1948) kama sababu ya mwachano huu, kanuni ya upekee na uwili-pacha inafafanua kuwa mchakato huu unalenga kupunguza ugumu wa kiutambuzi kwa kuunda maumbo pacha yenye upekee wa kimaana (Dressler, 1987).

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa mageuzi ya vitenzi katika Kinyakyusa si ya kinasibu, bali yanafuata kanuni asilia za kiisimu zinazolenga kuleta ulinganifu wa mfumo na upenyezi wa maumbo. Japokuwa kuna mwachano mkubwa katika baadhi ya vitenzi, uhifadhi wa sauti za asili katika vitenzi kama *-pa* (pa) na *lila* (lia) unathibitisha kuwa Kinyakyusa bado kimeshikilia kiini cha maumbo cha MB, huku kikirekebisha maumbo mengine ili kukidhi mahitaji ya kisasa ya mawasiliano.

**Uhifadhi wa Mofolojia ya Mame-Bantu katika Kinyakyusa**

Licha ya kuwapo kwa mageuzi makubwa ya kimofolojia ya msamiati wa msingi wa Mame-Bantu katika Kinyakyusa, kunadhihirika kuwapo kwa uhifadhi wa dhana ya mzizi wa maneno. Hii inamaanisha kuwa, kwa kiasi kikubwa dhana pamoja na umbo la mzizi wa maneno mengi ya Kibantu inarandana na ile ya Mame-bantu. Tazama mifano katika Jedwali Na. (5):

**Jedwali Na. 5: Uhifadhi wa Umbo la Mzizi wa Msamiati wa Msingi wa Mamebantu katika Kinyakyusa**

| Na. | Mame-Bantu | Maana | Kinyakyusa | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | *jʊ̀nì | ndege | i-n-juni | ndege |
| 2 | *bʊ́à | mbwa | i-mbwa | mbwa |
| 3 | *pépò | upepo | m-bepo/u-mbelo | upepo |
| 4 | *bʊ̀è | jiwe | i-li-bhwe | jiwe |
| 5 | *cèka | cheka | seka | cheka |
| 6 | *dɪ̀d | lia | lila | lia |
| 7 | *book | mkono | iki-bhoko | mkono |
| 8 | *(mu)– nywa /domo | mdomo | u-n-domo | mdomo |
| 9 | *jɪ̀mb | imba | imba | imba |
| 10 | *da | tumbo | palua-da | tumbo |

Data za Uwandani (2025)

Data katika Jedwali Na. (5) zinaonesha kwamba licha ya kuwapo mageuzi ya kimofolojia kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa, bado kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya maumbo ya mzizi wa maneno. Mathalani, *jʊ̀nì-juni, *bʊ́à-bwa, *pépò-bepo, *cèka-seka, *domo- domo, *pa-pa, *da-da, *ɪmb-imba na *íno-ino. Suala hili linathibitishwa na Dressler (2009) katika msingi wa pili wa NMA kwamba, kuna mahusiano ya uwili-pacha wa maumbo baina ya lugha zinazohusika. Uwili-pacha huo unaweza kuwa wa moja kwa moja au kufanana kwa baadhi ya nduni katika viambajengo vya mzizi wa neno. Mathalani, ufanano wa /*p, b*/ katika *pépò- bepo, /*b, β*/ katika *bʊ̀è-bhwe pamoja na /*d, l*/ *dɪ̀d-lila.

Philipo (2018) anaeleza kuwa /*p, b*/ zina uhusiano wa uwili-pacha katika namna au jinsi ya utamkaji (sauti zote hizo ni vipasuo vizuio) na mahali pa matamshi (sauti za midomo). Pia, /*b, β*/ hutamkiwa sehemu moja (midomo) vivyo hivyo kwa /*d, l*/ ambazo zote ni sauti ghuni za ufizi. Kwa mujibu wa M'Ngaruthi (2022), kudhohofika au kuimarika kwa baadhi ya sauti hizo za Mame-bantu katika lugha nyingi za Kibantu kunasababishwa na utiaji wa nguvu kimakusudi katika uzungumzaji au uharaka katika utamkaji wa baadhi ya sauti. Pasina shaka masuala hayo huweza kusababisha baadhi ya sauti kumezwa au kusikika tofauti wakati wa utamkaji na hatimaye kugeuza umbo asilia la neno.

Vilevile, tofauti hizo za kimasikizi zinaweza kusababishwa na msambao wa kijiografia, tajiriba ya jamii kuhusu hadhi ya msamiati pamoja na upekee wa lugha katika kujiundia sarufi yake tofauti na lugha nyingine zinazohusiana nayo (Guthrie, 1948; Christopher, 1967; Palome, 1975; BlytheI, & Croft, (2012; Booji, 2013). Kuhusu usarufishaji Booji (ameshatajwa) anafafanua zaidi kwamba, kutokana na Mame-bantu kutojitosheleza kisarufi hususani kifonolojia, wazungumzaji wa lugha nyingi za Kibantu kikiwamo Kinyakyusa wamejikuta wakipanua matamshi yanayoathiri siyo tu miundo bali, maana na hatimaye kusababisha mageuzi kamilifu ya umbo la msamiati wa msingi wa Mame-bantu. Sehemu inayofuata inafafanua zaidi kuhusu dhana ya mageuzi kamilifu ya kimofolojia kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa.

**Mageuzi Kamilifu ya Kimofolojia kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

Mageuzi kamilifu ya kimofolojia yanahusisha mabadiliko ya umbo zima la msamiati kutoka Mame-bantu kwenda Kinyakyusa. Hii inamaanisha kuwa, kuna baadhi ya maneno ya Mamebantu ambayo yamegeuzwa moja kwa moja kiasi cha kusababisha utofauti wa kiumbo baina ya lugha husika. Tazama mifano katika jedwali na (6):

**Jedwali Na. 6: Mageuzi Kamilifu ya Kimofolojia kutoka Mame-Bantu kwenda Kinyakyusa**

| Na. | Mame-Bantu | Kinyakyusa | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | *mʊ-kíla | imbikipiki | mkia |
| 2 | *jìj | gweisa | njoo |
| 3 | *njɪla | u-n-sebho | njia/barabara |
| 4 | *nti | m-piki | mti |
| 5 | *dʊ̀d | aka-jongo | nyongo |
| 6 | *jʊ́bà | u-rumu | jua |
| 7 | *jótò | i-fuku | joto |

Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. (6) linaonesha kwamba, kuna baadhi ya maumbo ya nomino za Mame-Bantu yamefanyiwa mageuzi kamilifu ambapo, umbo zima limegeuzwa kiasi cha kukosa uhusiano wa uwili-pacha baina ya Mamebantu na Kinyakyusa. Hii inaamaanisha kuwa maumbo husika yameshindwa kuhifadhika katika Kinyakyusa. Mattingly (1977) anaeleza kuwa, kuna nyakati katika maisha ya jamii yoyote msamiati huweza ama kubadilika au kupanuka kimaana na kiumbo. Hoja hiyo inaungwa mkono na Harya (2016) kwa kufafanua kwamba, mageuzi hayo hutokea taratibu kwa kuzingatia mabadiliko ya muundo na mfumo wa maisha ya jamii kama vile elimu, utamaduni pamoja na sayansi na teknolojia. Hivyo, suala la mageuzi kamilifu ya kimofolojia haliwezi kuelezwa kwa utabirifu bali, kwa kuhusianishwa na mageuzi ya jamii lugha husika. Hata hivyo, suala hili halijapata majibu thabiti kutoka kwa watafitiwa hivyo, linahitaji kuchunguzwa zaidi katika muktadha wa lugha za Kibantu ili kuweza kubaini sababu za msingi za kuwapo kwa mageuzi kamilifu ya kimofolojia kutoka Mame-bantu kwenda lugha nyingine za Kibantu.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Kwa kuzingatia mjadala na matokeo ya utafiti huu, inaweza kuhitimishwa kuwa mageuzi ya kimofolojia kutoka Kinyakyusa kwenda MB si mchakato wa kinasibu, bali ni mfululizo wa mabadiliko yenye mwelekeo mahususi wa kiisimu. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa michakato ya kimofofonolojia kama vile ulikwidishaji ukaakaishaji, uunganaji wa irabu, na udondoshaji wa konsonanti ndiyo chanzo cha mageuzi ya kimofolojia yaliyopo sasa katika lugha ya Kinyakyusa. Licha ya kuwapo kwa mageuzi hayo, Kinyakyusa kimebaki kuwa lugha hafidhina katika baadhi ya vipengele, hasa kwa kuhifadhi mizizi ya kale na sauti za kitambaza zinazosaidia kudumisha uhusiano wa kihistoria na MB. Aidha, kupitia kanuni za NMA, mageuzi haya yanatazamwa kama jitihada za lugha kuelekea kwenye uasili wa mfumo na uangavu wa kimofolojia. Hata hivyo, japokuwa michakato ya kimofofonolojia imegeuza baadhi ya vitamkwa vya MB, Kinyakyusa kimejirekebisha kimaumbo kwa kuongeza viambishi awali vya ziada katika nomino na vinyambulisho katika vitenzi ili kuimarisha ulinganifu wa mfumo na kurahisisha utambuzi wa maumbo ya lugha husika. Kwa hiyo, mageuzi haya yanapaswa kuchukuliwa kama ushahidi wa unyumbufu wa lugha katika kuimarisha upekee na uasili wake. Licha ya utafiti huu kutoa mwanga kuhusu mageuzi ya kimofolojia, tafiti zijazo zinaweza kujikita katika mageuzi na/au uhifadhi wa maana kupitia toni na miundo ya tungo kutoka MB kwenda lugha nyingine za Kibantu.

**Mapendekezo:** Inapendekezwa kuwa tafiti zijazo zijikite katika kuchunguza mageuzi ya kimofolojia katika lugha nyingine za Kibantu ili kuongeza uelewa wa mchakato wa kidayakronia na kubaini iwapo mifumo iliyobainika katika Kinyakyusa inajitokeza pia katika lugha nyingine. Pia, tafiti linganishi kati ya Kinyakyusa na lugha jirani kama Kisafwa, Kinyiha na Kimbindi zinaweza kufanyika ili kubaini kiwango cha ufanano na tofauti za kimofolojia zinazotokana na MB. Aidha, kuna haja ya kuchunguza uhusiano kati ya mageuzi ya kimofolojia, mabadiliko ya kimaana na kiimbo (toni) ili kuelewa kwa kina mwingiliano wa vipengele hivyo katika mabadiliko ya lugha.

**MAREJELEO**

BAKITA. (2022). *Kamusi kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.
Batibo, H. M. (1987). The Bantu ancestors' vision of the world. *Journal of Linguistics and Language in Education, 2*(1), 1–21.
Blythe, R. A., & Croft, W. (2012). How individuals change language. *PLoS ONE, 16*(6), e0252582. https://doi.org/10.1371/journal.pone.0252582
Blythe, R. A., & Croft, W. (2021). The role of language contact in linguistic evolution. *PLoS ONE, 16*(6), e0252582. https://doi.org/10.1371/journal.pone.0252582
Booij, G. (2013). Morphological change. In M. Aronoff (Ed.), *Oxford bibliographies in linguistics*. Oxford University Press.
Bostoen, K. (2007). Pots, words and the Bantu problem: On lexical reconstruction and early African history. *Journal of African History, 48*, 173–199.
Bostoen, K., & Bastin, Y. (2016). Bantu lexical reconstruction. In *Oxford handbooks online*. Oxford University Press.
Bostoen, K., de Schryver, G.-M., Guérois, R., & Pacchiarotti, S. (Eds.). (2022). *Reconstructing Proto-Bantu grammar*. Language Science Press. https://doi.org/10.5281/zenodo.7560552
Bostoen, K., & Guérois, R. (2022). Reconstructing suffixal phrasemes in Bantu verbal derivation. In K. Bostoen, G.-M. de Schryver, R. Guérois, & S. Pacchiarotti (Eds.), *Reconstructing Proto-Bantu grammar* (pp. 343–383). Language Science Press. https://doi.org/10.5281/zenodo.7575829
Batibo entry done above; next alphabetical continues:
Christopher, E. (1967). Cattle-keeping and milking in Eastern and Southern African history: The linguistic evidence. *Journal of African History, 8*(1), 1–17.
Creissels, D. (2009). Construct forms of nouns in African languages. In P. K. Austin, O. Bond, M. Charette, D. Nathan, & P. Sells (Eds.), *Proceedings of Conference on Language Documentation & Linguistic Theory 2* (pp. 73–82). SOAS.
Devos, M., & Bernander, R. (2022). Proto-Bantu existential locational construction(s). In K. Bostoen, G.-M. de Schryver, R. Guérois, & S. Pacchiarotti (Eds.), *Reconstructing Proto-Bantu grammar* (pp. 579–653). Language Science Press.
Dressler, W. U. (2003). Naturalness and morphological change. In B. D. Joseph & R. D. Janda (Eds.), *The handbook of historical linguistics* (pp. 461–471). Blackwell.
Dressler, W. U. (2009). Natural morphology. *Oxford Research Encyclopedia of Linguistics*. https://oxfordre.com/linguistics/view/10.1093/acrefore/9780199384655.001.0001/acrefore-9780199384655-e-576
Dressler, W. U., & Kilani-Schoch, M. (2016). Natural morphology. In A. Hippisley & G. Stump (Eds.), *The Cambridge handbook of morphology* (pp. 356–389). Cambridge University Press.
Dressler, W. U., & Kilani-Schoch, M. (2017). Natural morphology. In A. Hippisley & G. Stump (Eds.), *The Cambridge handbook of morphology* (pp. 356–389). Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/9781139814720.014
Dressler, W. U., Mayerthaler, W., Panagl, O., & Wurzel, W. U. (1987). *Leitmotifs in natural morphology*. John Benjamins.
François, A. (2016). The historical morphology of personal pronouns in northern Vanuatu. *Reconstruction et classification: Tendances actuelles, 47*, 25–60.
Guthrie, M. (1948). *The classification of the Bantu languages*. Oxford University Press.
Hamans, C. (2017). Language change and morphological processes. *Yearbook of the Poznań Linguistic Meeting, 3*, 1–23.
Harya, T. D. (2016). Language change and development: Historical linguistics. *Premise Journal, 5*(1), 103–117.
Heine, B., & Nurse, D. (2000). *African languages: An introduction*. Cambridge University Press.
Hyung-Soo, K. (1999). Universal phonological processes in eastern Bantu: A theoretical analysis. *Linguistics, 7*(1), 199–225.

Janda, R. D., & Joseph, B. D. (2003). On language, change, and language change. In B. D. Joseph & R. D. Janda (Eds.), *The handbook of historical linguistics* (pp. 3–180). Blackwell.

Juola, P. (2003). The time course of language change. *Computers and the Humanities, 37*, 77–96.

Knowles, G. (1997). *A cultural history of the English language*. Oxford University Press.

Kula, N. C., & Kadenge, M. (2015). Introduction: Phonetics and phonology in Bantu, Southern African. *Linguistics and Applied Language Studies, 33*(3), iii–v.

Maddison, I., Peter, L., & Sands, B. (1999). Clicks in East African languages. In R. Finlayson (Ed.), *African mosaic* (pp. 59–91). University of South Africa.

Maddison, I., & Sands, B. (2019). The sounds of the Bantu languages. In *The Bantu languages* (pp. 79–127). Routledge.

Maho, J. F. (2009). *NUGL online: The online version of the new updated Guthrie list*. https://brill.com/fileasset/downloads_products/35125_Bantu-New-updated-Guthrie-List.pdf

Mattingly, H. B. (1977). Vocabulary change and epigraphic dating. *Mnemosyne, 30*(1), 66–69.

Meeussen, A. E. (1967). Bantu grammatical reconstructions. *Africana Linguistica, 3*, 79–121.

Mndeme, S. M., & Ligembe, N. N. (2022). Phonological processes of Shambaa. *International Journal of English Literature and Social Sciences, 7*(3), 41–61.

Mukanda, A. (2022). A morpho-phonological analysis of Lwanga nouns and verbs. University of Nairobi.

Muzale, M. R. T., & Rugemalira, J. M. (2008). Researching and documenting the languages of Tanzania. *Language Documentation & Conservation, 2*(1), 68–108.

Nurse, D. (1983). History from linguistics: The case of the Tana River. *History in Africa, 10*, 207–238.

Nurse, D. (2008). *Tense and aspect in Bantu*. Oxford University Press.

Nurse, D., & Philippson, G. (Eds.). (2003). *The Bantu languages*. Routledge.

Persohn, B. (2017). *The verb in Nyakyusa: A focus on tense, aspect, and modality*. Language Science Press. https://doi.org/10.5281/zenodo.926408

Philippson, G. (2022). Double reflexes in north-western Bantu. In K. Bostoen, G.-M. de Schryver, R. Guérois, & S. Pacchiarotti (Eds.), *Reconstructing Proto-Bantu grammar* (pp. 25–58). Language Science Press.

Pozdniakov, K. (2018). *The numeral system of Proto-Niger-Congo*. Language Science Press.

Robinson, N. (2016). Word formation: The description of Nyakyusa derivation and inflection. *International Journal of Language and Linguistics, 3*(5), 62–71.

Siame, P., & Banda, F. (2024). Influence of morphophonological processes on the verbal structure of the Mambwe language. *ARRUS Journal of Social Sciences and Humanities, 4*(1), 29–37.

Sinnemäki, et al. (2024). A typological approach to language change in contact situations. *Diachronica HAL Open Science*, 1–35.

Van de Velde, M. (2019). The Bantu connective construction. In M. Van de Velde, K. Bostoen, D. Nurse, & G. Philippson (Eds.), *The Bantu languages* (2nd ed., pp. 1–13). Routledge.

Wills, J. (2022). Sorting out Proto-Bantu *j. In K. Bostoen, G.-M. de Schryver, R. Guérois, & S. Pacchiarotti (Eds.), *Reconstructing Proto-Bantu grammar* (pp. 59–101). Language Science Press. https://doi.org/10.5281/zenodo.7575817